<u>JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA</u>

# Ofisi Ya Rais

## Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa

## Halmashauri ya Wilaya ya Mvomero

Shule ya Sekondari Mzumbe

**NAMBA ZA SIMU:**
**Mkuu wa shule: 0717015950/ 0688687231**
**Makamu M/Shule: 0769831453/ 0713482594**
**Mwl wa Malezi: 0765440698/ 0625704268**

P. O. Box 19,
Mzumbe - Morogoro,
Tanzania.
Mzumbesecondarysch@gmail.com
**www.mzumbesec.sc.tz**

**TAREHE: 12.06.2023**

**MZAZI/MLEZI WA MWANAFUNZI,**

**…………………………………………………………………………….**
**S. L. P …………………………………………...............................**
**……………………………………………………………………………..**

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI MZUMBE HALMASHAURI YA WILAYA YA MVOMERO MKOA WA MOROGORO MWAKA 2023/2024**

1. Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika shule hii mwaka 2023/2024 na atasoma Tahasusi ya ……………….

   Shule ya **Sekondari Mzumbe ni shule ya Bweni ya Wavulana** ipo kilomita 25 kutoka **Morogoro Mjini** barabara ya kuelekea Iringa. Kama unatokea njia ya Dar es Salaam au Dodoma teremka stendi kuu ya mabasi **Msamvu**, panda daladala kuelekea stendi kuu ya mabasi madogo ya **Mafiga** kwa nauli ya shilingi 400/=, kisha panda daladala inayoelekea Mzumbe kwa nauli ya shilingi 1,000/=. Ukitumia Tax gharama yake ni T.Shs. 5,000/= kutoka Msamvu hadi **Mafiga**, na Tshs. 20,000/= kutoka **Mafiga** kwenda **Mzumbe**. Ukitokea njia ya Iringa teremkia eneo la **Sangasanga/ Njia panda Mzumbe**, ambapo unaweza kufika Mzumbe kwa daladala nauli yake haizidi shilingi 500/= au pikipiki kwa nauli ya shilingi 3,000/=.

   Muhula wa Masomo unaanza tarehe **14.08.2023**, hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe **13.08.2023** Mwisho wa kuripoti ni tarehe **31.08.2023.**

   **Mwanao atapokelewa shuleni akiwa na;**
   - ✓ Nakala (photocopy) ya "**Cheti cha Kuzaliwa"** na **"results slip" (Na Vyeti halisi kwa ajili ya Uhakiki)**
   - ✓ Kitambulisho cha **BIMA YA AFYA**
   - ✓ Amekamilisha mahitaji yote yapasayo kuja nayo kama maelekezo ya fomu hii.
   - ✓ Fomu ya Kupimwa Afya (Medical Examination) iliyojazwa na Mganga mkuu Hospitali ya serikali.
   - ✓ Amejaza Ahadi/Kiapo Cha Mwanafunzi.
   - ✓ Fomu ya **Malipo ya benki (Bank Pay Slip)** yalioainishwa kulipwa katika akaunti ya shule.
   - ✓ Fomu ya Utambulisho wa Mwanafunzi (**fomu hii itajaziwa shuleni baada ya mwanafunzi kufika).**

**NB: Mzumbe sekondari ni shule ya VIPAJI MAALUM kitaaluma, mwanafunzi atadhihirisha kuwa na kipaji hicho kwa kufaulu katika masomo yake yote.**

**KARIBU SANA KATIKA SHULE YASEKONDARI MZUMBE**

**Mbaraka M. Kupela**
**MKUU WA SHULE**

THE HEADMASTER
MZUMBE SECONDARY SCHOOL
P. O. BOX 19 - MZUMBE
MOROGORO

## 2. MAHITAJI MAALUM YA KUZINGATIA

### 2.1 SARE ZA SHULE

**(ZILIZOWEKEWA BEI UNAWEZA UKAZIPATA SHULENI KATIKA DUKA LA SHULE)**

(i) Suruali mbili (2) **Dark Blue.** (Kila moja Tshs. 20,000/=)
(ii) Suruali mbili (2) **Damu ya mzee** (Kila moja Tshs. 20,000/=)
(iii) Shati **Nyeupe** mbili (2) mikono mifupi. (Kila moja Tshs. 15,000/=)
(iv) T-Shirt mbili (2) za shule zenye kola. (Kila moja Tshs. 15,000/=)
(v) Track suit – **Blue Bahari moja** (1) (Tshs. 25,000/=)
(vi) Jezi ya michezo (Bukta na Fulana) Moja (1) **Blue Bahari**. (Tshs.12,000/=)
(vii) Sweta moja (1) **Blue** (Tshs. 15,000/=)
(viii) Soksi jozi mbili (2) **Nyeusi** (Tshs. 2,000/=)
(ix) Mkanda **Mweusi** wa Ngozi wa kuvalia suruali**.**
(x) Viatu vya shule ni **vyeusi** vya kufunga na kamba vyenye kisigino kifupi.
(xi) Viatu vya Michezo

### 2.2 VIFAA VYA USAFI

(i) Kwanja (1), Jembe lenye mpini (1), Reki (1), Soft broom (1), Hard broom (1), Squeezer (1), Brush ya kusafishia tundula choo (1). (**VINAPATIKANA KATIKA DUKA LA SHULE KWA GHARAMA NAFUU)**

### 2.3 MAHITAJI YA TAALUMA

(i) **Ream A4** ya karatasi mbili (2) kwa **mwaka** mzima. (**Double A/bright white multipurpose office paper)**

### 2.4 MICHANGO MBALIMBALI

| NA | AINA YA MCHANGO | KIASI (TSHS) |
|---|---|---|
| 1 | Mchango wa uendeshaji wa shule | 65,000/= |
| 2 | Tahadhari | 5,000/= |
| 3 | Nembo | 5,000/= |
| 4 | Kitambulisho cha shule | 5,000/= |
| | **JUMLA** | **80,000/=** |

Malipo haya yote yalipwe kwenye Akaunti ya shule;
**Namba ya Akaunti: 22101100075 NMB - The Headmaster Mzumbe Secondary School**

### 2.5 MAHITAJI YAKE BINAFSI YA BWENI

**(i) Godoro linakodishwa shuleni kwa gharama ya Tshs. 10,000 kwa Muhula.**
**(Ilipwe benki pamoja na michango mingine ya shule)**
(ii) Mashuka ya **Pink** jozi mbili (2), Blanketi (1), mto (1), chandarua nyeupe ya pembe nne (1) .
(iii) Taulo, vest nyeupe na nguo za ndani za kutosha.
(iv) Ndoo ndogo moja (1) (ya lita kumi)
(v) Kandambili kwa ajili ya kuogea
(vi) Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe)

### 2.6 MAHITAJI YAKE BINAFSI YA DARASANI

(i) Vitabu vya masomo ya tahasusi husika **(Orodha imeambatanishwa)**
(ii) Madaftari 12 (counter books), Scientific Calculator, Mathematical set, kalamu, penseli za kutosha na begi la kubebea daftari darasani.
(iii) “Dissecting Kit bag” kwa wanafunzi wa Mchepuo wa PCB.
(iv) “Laboratory coat” kwa wanafunzi wa Mchepuo wa PCB na PCM.

**NB: Mzazi utakapofika shuleni utakabidhiwa barua ya makubaliano ya wazazi inayoelezea mipango na mikakati ya kuunga mkono juhudi za serikali katika kuinua ufaulu na miundo mbinu ya shule.**

**3. SHERIA, KANUNI NA TARATIBU MUHIMU ZA SHULE**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

**SHERIA NA KANUNI ZA SHULE**

Sheria na kanuni hizi zinazingatia misingi ya HESHIMA, ADABU, UAMINIFU,UTII na TABIA NJEMA kwa ujumla

Wanafunzi wanatazamiwa kuwa mfano mzuri kwa heshima na tabia kauli na vitendo hivyo:

1. Mwanafunzi atasimama anapomsalimu mwalimu, mtumishi wa shule au mtu yeyote aliyemzidi umri
2. Hairuhusiwi kwa mwanafunzi kutumia lugha chafu 3ay a kihuni popote na wakati wowote hata kwa wanafunzi wenzake.
3. Hairuhusiwi kwa mwanafunzi
   (a) Kufuga kucha na nywele
   (b) Kufuga ndevu
   (c) Kunyoa kipara
   (d) Kutukana
   (e) Kutia dawa nywele (curly) na kujichubua ngozi ya mwili kwa madawa
   (f) Kuvaa vitu kama mapambo mfano Heleni, Mikufu bangili au vitu vya kiimani kama vile Rozali,
   (g) Kofia, Kanzu, Vilemba, Suruali fupi kwa kuwa Shule hii ni ya **Serikali**.
   (h) Kuvaa viatu vya soli nene na ndefu
   (i) Kuvaa kaptura na kandambili kwenye Bwalo la chakula na Ofisi zote za shule
   (j) Kuvaa suruali chini ya kiuno
   (k) Kuvaa nguo za mtindo, mfano- model
4. Mwanafunzi atasimama mstari wakati wa kupata huduma
5. Mwanafunzi atanyoosha mkono juu na kusimama anapouliza au kujibu swali
6. Anatakiwa kuwa mtulivu asipige kelele au vitendo vyovyote vitakavyo sababisha usumbufu kwa wengine anapokuwa Darasani Maktaba, bwenini, wakati wa kujisomea (prep) na katika mikusanyiko yoyote mfano paredi nk
7. Mwanafunzi **LAZIMA** awahi na ahudhurie mahali anapotakiwa katika shughuli za shule.Hivyo Mwanafunzi:-
   A. Aripoti shuleni tarehe ya kufungua shule na kujiandikisha rasmi siku na saa ya kuripoti kwa mwalimu anayehusika.
   B. Ahudhurie vipindi vyote darasani kama ilivyopangwa
   C. Ahudhurie kwenye kazi atakazopangiwa
   D. Ahudhurie kwenye paredi ya uhakiki wa uwepo wake shuleni (Roll call). Ukaguzi wa Usafi , kupandisha Bendera ya Taifa, Mikutano ya nyumba, Mikutano ya darasa na Maabara za shule.
8. **NI LAZIMA** mwanafunzi awe katika sare ya shule na awe na **KITAMBULISHO** kwa nyakati zote awapo shuleni na nje ya shule kama:-
   Anapotoka nje ya shule kwa ruhusa maalumu kwenda Posta, Kanisani, Msikitini, Benki, Hosipitali, likizo au kwa shughuli yoyote itakayomlamzimu kwenda nje ya shule.
9. **NI LAZIMA** mwanafunzi awe ndani ya mipaka ya shule wakati wote isipokuwa akiruhusiwa kuwa nje ya mipaka ya shule kwa ruhusa maalumu, na atapaswa kuwa na kibali (pass) cha maandishi.
10. Mwanafunzi lazima ahudhurie prep inayoanza saa 2.00 jioni na awe kitandani kwake wakati wa kuzima taa (lights out) saa 5:00 usiku.
11. Mwanafunzi haruhusiwi kutumia umeme kwa shughuli yoyote ile awapo bwenini au darasani.
12. Hairuhusiwi kufanya mikutano yoyote shuleni pasipo kibali cha Mkuu wa Shule na ikiwa kibali kimetolewa kikundi au chama kitatakiwa kuandika muhtasari wa kikao na nakala kuwasilishwa kwa Mkuu wa Shule.
13. USAFI: Mwanafunzi anawajibika kuwa msafi kwa mavazi na mwili wake na kushiriki kuyaweka mazingira ya shule katika hali ya usafi.
14. Mwanafunzi anapaswa kuvaa sare za Shule ya Sekondari Mzumbe muda wote akiwa ndani na nje ya shule na achomekee shati lake. **Mavazi yasiyo ya shule hayaruhusiwi kabisa.**
15. Hairuhusiwi kujihusisha na mikutano ya siasa katika kipindi chote awapo mwanafunzi.

16. **MAEENEO YASIYORUHUSIWA:**

Mwanafunzi haruhusiwi kufika/kuingia sehemu zifuatazo bila ruhusa maalumu:

a. Ofisi za shule
b. Bohari za shule
c. Kwenye disco, ngoma , mziki au kwenye sherehe yoyote ndani na nje ya shule
d. Maabara
e. Baa,kilabuni au mahali popote panapouzwa pombe au vileo vingine
f. Nyumba za wageni (Guest House)
g. Nyumba za watumishi/walimu

**ZINGATIA:**

Unataarifiwa kuwa shule hii ni shule ya Serikali wala siyo ya **DINI** Fulani. Aidha inazingatia katiba ya nchi kuhusu uhuru wa kuabudu, hivyo wanafunzi huruhusiwa kwenda sehemu za ibada kulingana na imani zao. Pia kumepangwa vipindi viwili vya dini katika ratiba ya masomo kwa siku ya Jumatano na kila siku jioni kabla ya chakula kuanzia saa 12.00 – 01.00 usiku. Wanafunzi hawaruhusiwi kuanzisha ratiba yao ya kuabudu katikati ya vipindi na ratiba zingine za shule. **Tofauti ya hayo Mzazi/Mlezi anashauriwa kumtafutia mwanafunzi shule ya seminari endapo mwanafunzi huyo ana wito wa dini husika**.

## MAKOSA YANAYOWEZA KUMFUKUZISHA MWANAFUNZI SHULE:

1. Wizi
2. Uasherati, ushoga na ulawiti,ubakaji
3. Ulevi wa aina yoyote kama utumiaji wa madawa ya kulevya, pombe, sigara,bangi, mirungi n.k
4. Makosa ya jinai
5. Kuoa au kuolewa
6. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
7. Kupigana au kumpiga mwingine.
8. Kudharau Bendera ya Taifa
9. Kulala nje ya shule bila ruhusa ya Mkuu wa shule
10. Kuchochea au kufanya vurugu, kugoma kwa namna yoyote
11. Kutoa lugha ya matusi
12. Kumdharau kiongozi wa shule, mwalimu, mfanyakazi na jamii kwa ujumla
13. Kutohudhuria vipindi
14. Mwanafunzi kumiliki **simu** au sehemu ya simu **kama laini, Charger nk**
15. Kupata wastani wa alama chini ya **60%** katika masomo yake
16. **Kukosa kuhudhuria vipindi darasani na au kutofanya mitihani na majaribio kwa makusudi**

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

**President's Office,**

**Regional Administration and Local Government**

**Mvomero District Council**

Mzumbe Secondary school

**Mobile Phone:**
**Headmaster: 0717015950/ 0688687231**
**SecondMaster: 0769831453/ 0713482594**
**Patron: 0765440698/ 0625704268**

P. O. Box 19,
Mzumbe - Morogoro,
Tanzania.
Mzumbesecondarysch@gmail.com
**www.mzumbesec.sc.tz**

# MEDICAL EXAMINATION FORM FORM

**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION OF ………………………………………………………... FORM V……**

Please examine the above named as to his fitness for admission to school as a student.

***Name and signature of requesting Officer.***

Name ……………………………………………….. Signature ……………………………..

Date ……………………………………………

**To be completed by a Government Medical Officer in respect of FORM 1/5 entrants:**
**Pupil's Full Name……………………………………………………………………………………………………………………**

**Blood count (Red and White) ……………………………………………………………………………………………**

**Stool Examination ………………………………………………………………………………………………………………**

**Urinalysis…………………………………………………………………………………………………………………………**

**Syphilis Test………………………………………………………………………………………………………………………**

**T. B. Test……………………………………………………………………………………………………………………………**

**Eye Test………………………………………………………………………………………………………………………………**

**Ears……………………………………………………………………………………………………………………………………**

**Chest…………………………………………………………………………………………………………………………………**

**Spleen………………………………………………………………………………………………………………………………….**

**Abdomen……………………………………………………………………………………………………………………………**

**Blood Group…………………………………………………………………………………………………………………………**

**ADDITIONAL INFORMATION: e.g. Physical defects or impairments infections, chronic or family diseases etc.**

……………………………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………………………

I have examined the above named and I consider that he is physically fit/unfit to pursue as stated above.
Name and signature of Certifying Officer.

Name ………………………………………… Signature………………………………………
Station ………………………………………… Designation …………………………………..
Date ……………………………………… STAMP ………………………………………

## AHADI/ KIAPO CHA MWANAFUNZI

Mimi ………………………………………………………………………………KIDATO CHA 5 …………
Ambaye nimechaguliwa kujiunga na **SHULE YA SEKONDARI MZUMBE KIDATO CHA 5** mwaka 2023 /2024 ninaipokea na kuikubali nafasi niliyo pewa kwa malengo ya kusoma kwa bidii na kufikia malengo ya Taifa na Shule ya Sekondari ya Mzumbe.

Ninatambua kuwa nafasi hii ni adimu, nyeti na ya upendeleo kwangu ili niweze kusoma na kufanya vizuri katika masomo nikiwa na tabia na mwenendo mwema kwa ajili ya taifa langu la Tanzania, familia yangu na kwa ajili yangu pia.

Nina amini kuwa vitendo vyovyote vinavyopelekea uzembe katika kufanikisha makusudio haya ni hujuma kwa Taifa langu, familia yangu na kwangu pia. Hivyo ninaahidi kuwa, nikiwa hapa shuleni:

(i) Nitasoma kwa bidii kwa malengo ya kufanya vizuri katika masomo yangu.
(ii) Nitashika na kufuata sheria na taratibu zote za shule kama nilivyo zisoma na kuzielewa na zingine zitakazo kuwa zikitolewa mara kwa mara.
(iii) Sitajihusisha na vitendo vyovyote vya utovu wa nidhamu nikiwa hapo shuleni.
(iv) Nitafaulu kaika mitihani yangu yote na kamwe sitapata chini ya alama za ufaulu za shule ambazo ni 60%
(v) Ikiwa nitakiuka sheria kanuni na taratibu za shule kama nilivyo zisoma na kuzielewa, nitakubali kurudi nyumbani kumwita mzazi/ mlezi wangu. …………………………………………………… ( Jina la mzazi) kwa ajili ya hatua zaidi.

Saini ya mwanafunzi …………………………………… tarehe ……………………………………………………

---

## SEHEMU YA MZAZI/MLEZI

Mimi ………………………………………………… ninakubali mtoto wangu ……………………………………………………
Kupata na kupokea nafasi katika shule ya sekondari Mzumbe mwaka 2023. Ninaahidi kumpatia mahitaji yote ya shule kama ilivyo katika maagizo ya kujiunga na shule. Ninakuhakikishia kuwa nitashirikiana na shule wakati wote kuona kuwa mwanangu anatekeleza wajibu wake kwa shule na kwa taifa, ikiwa ni pamoja na kufanya vizuri katika masomo.

Anuani yangu ya kudumu ni ………………………………………………………………..

………………………………………………………………..

Simu ………………………………………………………

Saini ya Mazazi/Mlezi ………………………………………Tarehe ………………………….

**NB:** **Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule : 0717015950/ 0688687231**
- **Makamu Mkuu wa Shule: 0769831453/ 0713482594**
- **Mwandamizi Taaluma: 0763185923/ 0658821783**
- **Mwandamizi Malezi: 0765440698/ 0625704268**

# ORODHA YA VITABU

## PHYSICS BOOKS

1. Tanzania institute of education (TIE), Physics for Advanced Level Secondary Schools Student's Book Form 5
2. Tanzania institute of education (TIE), Physics for Advanced Level Secondary Schools Student's Book Form Six.
3. Muncaster Rogers, (1993) A level physics 4$^{th}$ Ed, Nelson Thorns Ltd, U.K.
4. Principles of physics class XI.
5. Principles of physics class XII.
6. Tom Duncan

## CHEMISTRY BOOKS

1. Tanzania Institute of Education (TIE), General Chemistry for Advanced Level Secondary Schools Form F5 & 6
2. Tanzania Institute of Education (TIE), Organic Chemistry for Advanced Level Secondary Schools Form F5 & 6
3. Tanzania Institute of Education (TIE), Physical Chemistry for Advanced Level Secondary Schools Form F5 & 6
4. Tanzania Institute of Education (TIE), Inorganic Chemistry for Advanced Level Secondary Schools Form F5 & 6
5. Ramsden. E.N, (2000), A – Level Chemistry, 4$^{th}$ Ed, Cambridge University Press London
6. Mkayula, L.L et al (1998), Physical Chemistry, Vol. 1 (Mzumbe Book Project), Mzumbe Tanzania.
7. Jain. S. K (2010), Conceptual Chemistry For class xi, S. Chand & Company Ltd, New Delhi, India.

## BIOLOGY BOOKS

1. Taylor D.J. Biological Science 1&2, 3$^{rd}$ Ed, Cambridge University Press, London.
2. Tanzania Institute of Education (TIE), Biology for Advanced Level Secondary Schools Student's Book Form 5
3. Tanzania Institute of Education (TIE), Biology for Advanced Level Secondary Schools Student's Book Form Six.
4. H.G.Q, Rowett, Guide to Dissection.
5. Michael Kent, Advanced Biology, Oxford University Press.
6. Understanding Biology for Advanced Level

## ADVANCED MATHEMATICS BOOKS

1. Tanzania Institute of Education (TIE), Advanced Mathematics for Advanced Level Secondary Schools Student's Book Form Five.
2. Tanzania Institute of Education (TIE), Advanced Mathematics for Advanced Level Secondary Schools Student's Book Form Six.
3. Sillem, Advanced Mathematics Form Five.
4. Sillem, Advanced Mathematics Form Six.

## HISTORY BOOKS

1. UNESCO General History of Africa Vol 1-7
2. Major Events of African History, Kamara Mwijage
3. African from 5 to 12th century
4. African under Colonial Dominion 1880-1935
5. History for Advance Level TIE books (Form V & 6)
6. Mastery World History Vol 3 -7 by Norman Lowe
7. European History since 15th century
8. World History Vol 3-10

## GEOGRAPHY BOOKS

1. Current Or New Tie Advanced Book Physical Geography
2. Current Tie Advanced Book Human Economic Geography
3. Current Tie Advanced Book Practical Geography
4. Human Economic Geography By Mogarn
5. Practical Geography By Prichard And Zist Kamili
6. Physical Geography Monkhouse, Msabila, Zits Kamili
7. Geography NECTA Review

**ENGLISH LANGUAGE BOOKS**

1. Advanced level English Language : Oxford.
2. Betrayal in the City – Francis Imbuga
3. I Will Marry When I Want – Ngungi wa Thiong'o & Ngungi wa Mirii.
4. An Enemy of the People.
5. The Beautifu; Ones are not Yet Born – Ayi Kwei Armah
6. A man of the People – Chinua Achebe
7. Divine Providence – Severine N. Ndunguru.